- Mtamba akiwa na mimba ya miezi 8 -9 azoeshwe eneo la kukamulia kwa kuoshwa kiwele na kupewa vyakula vya ziada.
- Kwa kipindi cha masaa machache kabla ya kuzaa huonyesha dalili za kuwa na wasiwasi, hamu ya chakula kupungua kutembea kwa shida na kutazama nyuma. Huangaika ovyo, kupiga kelele, na kutoa majimaji meupe sehemu ya uke.
- Kwa kawaida ng'ombe hubeba mimba miezi tisa lakini aweza kuwahi au kuchelewa kuzaa kwa siku 10 kutokana na sababu mbali mbali.

## UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU

Ni muhimu sana kwa mfugaji kutunza kumbukumbu maana kutamfanya kuwa na taarifa za matukio muhimu ya ng'ombe wake yaliyopita Mfano:- *Kuzaa , Kutibiwa, kukaushwa , idadi ya maziwa aliyotoa na nyinginezo*

## FAIDA ZA KUMBUKUMBU KATIKA NG'OMBE WA MAZIWA

- Kutambua ng'ombe wenyekuleta faida na wenye matatizo katika zizilake; hii itamsaidia mfugaji kufanya maamuzi yanayostahili
- Kujua endapo anapata faida au hasara katika ufugaji wake.
- Kutambua maendeleo kwa ujumla.

## KUZUIA MAGONJWA

- Mfugaji anashauriwa kuzuia uwezekano wa magonjwa kuingia katika mifugo yake
- Kupunguza chimbuko la magojwa kama vile maji machafu, zizi chafu, nyasi zilinazohisiwa kuwa na wadudu wa naoweza kuambukiza magonjwa.
- Ng'ombe wa kutoka zizi lingine wachunguzwe kwanza kabla ya kuchanganywa na ng'ombe walio katika zizi lingime.
- Kuogesha ng'ombe kwa kutumia dawa ya kuuwa ( Kuondoa ) Kupe kutokana na ushauri wa mtaalamu wa mifugo
- Kupewa dawa za mimyoo kwa kufuata ushauri wa mtaalam wa mifugo
- Kuwapa chanjo mbali mbali ili kuzuia magonjwa
- Mtamba atibiwe mapema pindi anapougua.


Kwa ushauri zaidi onana au mwandikie
Mkuu wa Idara

Kitivo cha kilimo
Idara ya sayansi wanyama na uzalishaji
P.O.Box 3004,
Morogoro, Tanzania

*Tel.: 255-23-2604617*
*Fax: 255-23-2604562 E-Mail:*
*dasp@suanet.ac.tz; www.suanet.ac.tz*

# SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE (SUA)

# UFUGAJI BORA WA NG'OMBE WA MAZIWA (MITAMBA)



## UTANGULIZI

Ng'ombe wa maziwa waliopo nchini Tanzania ni wa jamii ya

- **FRIESIAN**
- **ARYSHIRE,**
- **JERSEY,**
- **CHOTARA.**

Jamii ya **FRIESIAN** na **ARYSHIRE** wanapatikana SUA

Hawa ni Ng'ombe wa kisasa wenye uwezo wa kukua haraka na kutoa maziwa mengi wakilinganishwa na ng;ombe wa Asili ( Kienyeji)

## MAMBO MUHIMI YA KUZINGATIA KATIKA UFUGAJI BORA WA NG'OMBE WA MAZIWA

- Kujenga Banda imara na Safi
- Utunzaji bora wa ng;ombe wa maziwa
- Ulshaji bora
- Uzuija wa mangonjwa
- Kuweka kumbukumbu sahihi

## BANDA BORA LA NG'OMBE WA MZIWA

- Banda lisijengwe kuelekea unakotoka upepo.
- Sakafu iwe imara isiyoteleza na yenye mwinuko upande mmoja ili kurahisisha usafirishaji, ijengwe kwa mawe na kusakafiwa kwa saruji au kusindiliwa kwa udongo.
- Kuta zijengwe kwa nguzo za miti au mabanzi na fito kuruhusu hewa yakutosha kupita.
- Paa liwe imara lisivuje. Lawezakuezekwa kwa bati, nyasi au makuti

## UTUNZAJI WA NG'OMBE WA MAZIWA ( MITAMBA)

Kipindi cha utunzani wa mitamba kimegawanyika katika sehem kuu mbili

- Kutoka kuachisha kunyonya hadi kupandisha mara ya kwanza
- Kutoka kupandizwa mara ya kwanza hadi kuzaa

Vipindi vyote viwili ni vya muhimu kuzingatiwa ili kuhakikisha kwa muda unaotakiwa na kwa gharama ndogo yenye kuleta mapato makubwa katika mzao wake wa kwanza

## CHAKULA KIKUU CHA NG'OMBE WA MAZIWA

Chakula cha ng'ombe ni majani, mtamba anatakiwa alishwe majani bora ili awe naafya nzuri lakini ni muhimu pia kumpa chakula cha ziada hasa wakati wa upungufu wa majani ( Kiangazi). Chakula hicho ni lazima kiwe na mchanganyiko wa protin, wanga na nadini au chumvichumvi mfano :-

- **Proteini:-** *Mashudu ya pamba, Alizeti, Ufuta, Majai ya lukina.*
- **Wanga:-** *Pumba za Mahindi, Ngano, Mpunga n.k*

Vyote vichanganywe katika uwiano wa 2 wanga na 1 protini na isizidi asilimia 5 ya madini

- Mtamba apewe kilo mbili ya mchanganyiko huo kwa siku. Kufanya hivi mfugaji ataepuka utapimlo wa mtamba. Katika kipindi cha mtamba kupewa chakula cha ziada ni muhimu apewe majani ya kutosha
- Mtamba apewe maji safi na ya kutosha
- Usimbadilishie ratiba na mfumo wa chakula ghafla

*Kimetayarishwa na Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo*
*Dr. N. Madalla*
*Prof. N. Urio*
*Miss. Grace Ngomalilo*
*Mr.* Khaji Mkata

Kwa ushauri zaidi onana au mwandikie
Mkuu wa Idara

Kitivo cha kilimo
Idara ya sayansi wanyama na uzalishaji
P.O.Box 3004,
Morogoro, Tanzania

***Tel.: 255-23-2604617***
***Fax: 255-23-2604562 E-Mail:***
***dasp@suanet.ac.tz; www.suanet.ac.tz***

## FAIDA ZA UTUNZAJI BORA WA NG'OMBE ( MTAMBA)

- Mtamba anakuwa an afya nzuri n inakuwa vigumu kushambuliwa na magonjwa mbalimbali.
- Mtamba huwezakukua haraka na kufikia uwezo wa kupandwa mapema. Kuanzia kilo 250 uzito huu utamwezesha kukua vizuri pia kuepuka matatizo ya kushindwa kuzaa
- Mtamba anakuwa na afye nzuri anayeweza kutoa maziwa mengi na kwa muda mrefu
- Gharama za matibabu zinapungua

## UZALISHAJI WA NG'OMBE WA MAZIWA ( MITAMBA)

- Mtamba atakuwa tayari kupandishwa kama kawaida kila daada ya siku 21 wastani.
- Mtamba apandishwe kwa kutumia dume au uhamishaji anapofikisha umri wa miezi 18—24 na kilo 250kgs—300 kgs
- Ina wezekana mtamba kutoshika mimba baada ya kupandishwa uwe mwangalifu kuendelea kuchakuza dalili zozote za joto.
- Baada ya mtamba kupandwa, tafuta huduma ya mtaalam wa mifugo ili apime mimba miezi miwili tka kupandwa.
- Mtamba anapokuwa na mimba ya miezi saba alishwe kilo mmoja ya mchanganyiko wa chakula cha ziada , na baadaye akiwa na mimba ya miezi 8—9 apewe kilo mbili